

UNABII

Milenia: Mambo Muhimu 8 Unayopaswa Kufahamu

Karibu tusafari pamoja katika unabii unaofunua nyakati muhimu katika mpango mkubwa uliowekwa na Mungu – kipindi cha miaka elfu moja, kinachojulikana kama "mileniam."...

PR. ALMODAD AMOS YARAGWILLER

2026

Karibu tusafari pamoja katika unabii unaofunua nyakati muhimu katika mpango mkubwa uliowekwa na Mungu – kipindi cha miaka elfu moja, kinachojulikana kama "mileniam." Ingawa neno hili halipatikani katika kurasa takatifu za Maandiko, mafunuo ya Mungu yanaliweka wazi jambo hili la pekee, na lenye umuhimu mkubwa katika mtiririko wa matukio makuu ya historia ya dunia hii na katika kuanzishwa kwa ufalme wa Mungu utakaodumu milele.

Milenia tunayoizungumzia hapa, ni kipindi maalum cha miaka elfu moja, kilichotabiriwa katika Biblia, kinachoanza mara tu baada ya kuja kwa mara ya pili kwa Yesu Kristo. Katika kipindi hiki, wenye haki waliofufuliwa au kunyakuliwa wanakuwa pamoja na Kristo mbinguni, wakati waovu wakibaki wamekufa katika makaburi yao kwenye dunia iliyo ukiwa. Katika kipindi hiki adui mkuu, ambaye ni Shetani, amefungwa kwenye dunia iliyojaa ukiwa, hana uwezo wa kudanganya watu tena. Kipindi hiki kinatupeleka katika matukio ya mwisho ya hukumu, ufufuo wa waovu, uasi wa mwisho wa Shetani, na uumbaji wa mwisho wa mbingu mpya na nchi mpya.

Fufuo Kuu Mbili Zitakazotoea

Maandiko Matakatifu yanasema kuhusu wakati ambapo wote walioko makaburini watasikia sauti Yake na kutoka nje. Kuna ufufuo mbili: mmoja kwa ajili ya uzima, na mwingine kwa ajili ya hukumu (Yohana 5:28, 29).

Ufufuo wa Uzima: Huu utatokea wakati wa kuonekana kwa Bwana akiwa katika utukufu (1 Thesalonike 4:16). Wale waliokufa katika imani watafufuliwa, na kwa pamoja wakiwa na waaminifu waliosalia wakiwa hai, wananyanyuliwa kuwa pamoja na Bwana angani. Wanapanda

kwenda kuishi Naye mbinguni kwa miaka elfu moja (Ufunuo 20:5, 6). Ikiwa waliofufuliwa kwanza ni wale waaminifu na watakatifu wa Mungu, basi waliosalia ni kundi la watu ambao walikufa kabla ya kufanya toba ya dhambi. Hawa wafu waliosalia, yaani waliokufa katika uovu hawataishi tena hadi miaka elfu moja itakapokwisha (Ufunuo 20:5). Ikiisha hiyo ndipo watakapofufuliwa ili waweze kuhukumiwa.

Ufufuo Maalum

Wakati wote walilala (waliokufa) katika imani wanafufuka wakiwa na miili isiyoweza kuona uharibifu tena, na wakati wanamlaki Mungu katika mawingu angani, ni katika wakati huo huo, “hao pia waliomchoma” wanafufuliwa kumtazama Yesu akiwa katika utukufu Wake na kuiona heshima iliyowekwa juu ya waaminifu na watiifu wa Mungu (Ufunuo 1:7). Hawa waliomchoma ni “wale waliomdhihaki na kumdharau Kristo katika wakati wa mateso Yake, ni pamoja na wale wapinzani wakuu zaidi wa kweli Yake na wakuu wa watu Wake, hao wanafufuliwa kumtazama Yeye katika utukufu Wake, na kuona heshima iliyowekwa juu ya waaminifu na watiifu.” ~ (Ellen G. White Impending Crisis p.30.1).

Ufufuo huu maalum ni sehemu ya utimilifu wa ahadi ambayo Yesu alitoa katika tukio fulani wakati wa mateso Yake (Mt. 26:63–64). Wakati Yesu akiteswa na kuhukumiwa, kuhani mkuu Kayafa alidhihaki akisema, “Tuambie kama wewe u Kristo, Mwana wa Mungu.” Yesu alijibu, “Wewe wasema,” na akaongeza, “Lakini nawaambia .... mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, na akija katika mawingu ya mbinguni.”

Hatima ya Wasiojiweka Tayari

Kwa wale watakaokuwa hai duniani wakati wa kuja kwa Bwana, lakini ambao maisha yao hayapatani na mapenzi Yake, uharibifu unawangoja. Waovu walio hai watauawa kwa utukufu wa kuja Kwake na kwa upanga utokao kinywani Mwake (2 The. 2:8; Yer. 25:30-33; Ufu. 19:17, 18; Yer. 16:4).

Ukiwa wa Dunia

Baada ya hukumu hii, dunia inaachwa katika hali ya uharibifu mkubwa. Nabii anaielezea hali kama ukiwa na tupu, bila mtu yeyote anayeishi ndani yake, na mbingu zikiwa giza (Yer. 4:23-27). Ni tukio la ukiwa mkuu.

Kufungwa kwa Adui

Katika kipindi hiki cha miaka elfu moja, yule joka, yule nyoka wa zamani, aitwaye Ibilisi na Shetani, anawekwa katika kifungo. Malaika anashuka kutoka mbinguni, akiwa na ufunguo wa shimo lisilo na mwisho na mnyororo mkuu mkononi mwake. Anamshika Shetani na kumfunga kwa miaka elfu, anamtupa katika shimo, na anaweka muhuri juu yake ili asiwadanganye mataifa tena mpaka ile miaka elfu itakapotimia (Ufu. 20:1-3). Andiko pia linaonyesha malaika waliokosa nao wanawekwa katika kifungo hiki chenye giza wakiingoja hukumu ya siku ile kuu (2 Pet. 2:4). Hali hii ya dunia, iliyo ukiwa na giza, inaweza kueleweka kama "shimo lisilo na mwisho" la maono ya kiunabii (Isa. 24:19-22).

Wakati wa Kusubiri

Kwa miaka hii elfu, wenye haki watakuwa pamoja na Kristo mbinguni, wakitawala pamoja Naye (Ufu. 20:4, 6). Ingawa urithi wao wa mwisho ni kurudi hapa duniani (Mt. 5:5), makao yao ya sasa ni ya mbinguni. Waovu wanabaki wamekufa makaburini mwao (Isa. 24:22; Ufu. 20:5). Shetani amefungwa katika dunia iliyo na ukiwa, hawezi kudanganya. Dunia yenyewe inabaki ukiwa na tupu (Yer. 4:27), ikiadhimisha Sabato ndefu ya pumziko baada ya karne nyingi za shughuli za wanadamu na dhambi (linganisha 2 Nya. 36:21; Law. 26:33-35).

Kuangamizwa na Shetani na Waovu

Mwishoni mwa miaka hii elfu moja, matukio muhimu yanatokea. Yohana katika maono aliuona mji mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka kwa Mungu mbinguni, umetayarishwa kama bibi arusi aliyepambwa kwa mumewe (Ufu. 21:2).

Mji huu unashuka duniani. Nabii anaelezea kuwa Mungu atatengeneza ambao nabii anauita Mlima wa Mizeituni, mlima huu utapasuka katikati, na bonde kubwa linaundwa, likitoa mahali pa mji Yerusalemu kutua na kutulia (Zek. 14:4, 5).

Mwishoni mwa miaka elfu, Shetani anafunguliwa kutoka katika kifungo chake cha ukiwa (Ufu. 20:7). Hii inatokea wakati waovu wanapofufuliwa kutoka makaburini mwao (Ufu. 20:5).

Akiwa amefunguliwa, Shetani anatoka kuwadanganya mataifa yaliyo katika pembe nne za dunia, Gogu na Magogu, kuwakusanya pamoja kwa vita. Hawa wanaizunguka kambi ya watakatifu, na mji uliopendwa

(Yesusalemu). Lakini moto unashuka kutoka kwa Mungu mbinguni na kuwateketeza (Ufu. 20:8, 9). Hii ndio mauti ya pili (Ufu. 20:14).

Uumbaji Mpya

Baada ya uharibifu wa waovu, Mungu analeta uumbaji mpya. Andiko linaahidi mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki inakaa ndani yake (2 Pet. 3:10-14). Hii inakuwa makao ya milele ya hao waliokombolewa.

Hitimisho

Wakati Mungu anapotufunulia mambo yanayohusu nyakati zijazo, ni kwa sababu anapenda kuona wote tukijiandaa kwa uzuri na wote tukiokolewa. Inaleta maana zaidi kufanya maamuzi ya kumpokea Mungu leo na sasa hivi, ili wakati maisha haya yatakapokoma uweze kuwa miongoni mwa wale watakaokuwa katika aidha ufufuo wa kwanza, au wale watakaokutwa wakiwa hao na wakiwa waaminifu. Muda hauko mbali sana, dunia hii itakutana na hukumu ya Mungu, na Shetani atakatiliwa mbali, wanaompokea Yesu leo na kufanya toba ya dhambi sasa, wanajiweka katika upande salama, upande wa Mungu, upande wa wale watakaokombolewa na kuitumia miaka hii elfu moja pamoja na Bwana, na kisha kuishi naye Milele na milele hapa duniani.

Zaidi kutoka Injili Milele

Makala, vitabu, video na sauti zaidi zinapatikana kwenye maktaba ya Injili Milele:

Je, Sabato Ilikoma kwa Kuwa Ilikuwa Kivuli cha Mambo Yajayo?
Sabato · PDF

Sanduku la Agano: Je, Litaonekana Tena?
Unabii · PDF

Nini Hasa Maana ya Kibiblia ya Maneno ya Baba: “Mimi Leo Nimekuzaa”?
Uungu · Video

Je, Yesu ni “Mungu Mwana” au “Mwana wa Mungu”?
Uungu · Video

Kwa Nini Mungu Alimuumba Lusifa?
Pambano Kuu · PDF

Papa Gregory XIII Alipobadilisha Kalenda: Siku Zilivurugwa, Sabato Ilipotea?
Sabato · PDF

Injili Milele

almodad-2.github.io/injili-milele/sw/

WhatsApp +255 718 834 621 · modaofhope@gmail.com

© 2026 Pr. Almodad Amos Yaragwiller · Injili Milele. Haki zote zimehifadhiwa. Usiuze nakala hii bila ruhusa ya maandishi ya mwandishi.